



**COUNTY ASSEMBLY OF MOMBASA
THE HANSARD**

Wednesday, 8th February, 2023
Third Assembly – Fourth Sitting

*[The County Assembly met at 2:50p.m. at the County Assembly Buildings]
[The Temporary Speaker (Hon. Amriya Boy Juma) in the Chair]*

PRAYERS

The Temporary Speaker (Hon. Amriya Juma): Honourable Members, you may be seated. Yes Clerk?

PAPER

REPORT ON THE INDUCTION WORKSHOP FOR MEMBERS OF THE THIRD COUNTY ASSEMBLY OF MOMBASA HELD FROM 30th OCTOBER, 2022 TO 7th NOVEMBER, 2022 AT OLE SERENI HOTEL, NAIROBI COUNTY

Yes, Honourable Athman Mwamwiri, the Leader of Majority Party please lay the Paper.

The Leader of Majority Party (Hon. Mwamwiri): Thank you Madam Speaker. I wish to lay Paper, Report on the induction training for Members of the Third County Assembly of Mombasa held from 30th October, 2022 to 7th November, 2022 at Ole Sereni Hotel, Nairobi County. Thank you.

The Temporary Speaker (Hon. Amriya Juma): Thank you Honourable Mwamwiri. Yes Clerk?

PAPER

REPORT ON THE INDUCTION TRAINING OF THE COMMITTEES ON APPOINTMENTS, HOUSE BUSINESS AND SELECTION HELD FROM 10th TO 12th NOVEMBER, 2022 AT SUN N SAND BEACH RESORT, KILIFI COUNTY

The Temporary Speaker (Hon. Amriya Juma): Yes, Honourable Athman Mwamwiri?

The Leader of Majority (Hon. Athman Mwamwiri): Thank you Madam Speaker. I wish to lay a Paper, Report on the induction training of the Committees on Appointments, House Business and Selection held from 10th to 12th November, 2022 at Sun n Sand Beach Resort, Kilifi County. Thank you.

The Temporary Speaker (Hon. Amriya Juma): Thank you Honourable Mwamwiri. Yes Clerk?

MOTION

[Resumption of Business interrupted during the Third Sitting]

PREVENTIVE AND MITIGATION MEASURES AGAINST CANCER, LIFESTYLE AND OTHER MALIGNANT DISEASES

Resumption of Business from Wednesday 8th February, 2023 at 10:00a.m during the Third Sitting. Honourable Members, the Motion by Honourable Juma Mwalimu on preventive and mitigation measures against cancer, lifestyle and other malignant diseases was moved during the Third Sitting of this House, unfortunately due to power outage it could not be finalized. So Honourable Members those who had not made their contributions can now do so, thank you the floor is open. Yes, Honourable Hamida?

Hon. Noor: Thank you Madam Speaker. As you are well aware especially in Mombasa, we have breast cancer. My colleague has stated that he needs awareness in all Wards in Mombasa County which I support in the Motion; this will give us priority to our people so that they can have the privileges of going to check the cancer disease in the early stage. Honourable Speaker during the morning session, there is one of my colleagues who said that mental health should even be included in this. Madam Speaker, you are aware that last term we had a Motion on mental health which was brought by me and it went through the House and it did not go further than that. We did not implement it and you are all aware that Covid-19 has really affected us as a County in our businesses and in our economy. So, with that I do urge this Assembly so that we can continue to spearhead the mental health Motion so that it can take place and it can be accepted as Bill so that we can do it well with the County in our County, with that I do support the Motion. Thank you.

The Temporary Speaker (Hon. Amriya Juma): Thank you Honourable Hamida. Yes, Honourable Patrick.

Hon. Mbelle: Ahsante Bi. Spika kwa kunipa fursa hii. Kwanza nimpongeze aliyeleta mada hii ndani ya Bunge kwakuwa aliolileta ni jambo la maana kwa sababu wengi wetu kama wajua umetoka nyanjani mara nyingi simu haziishi kuita kutokana na sana sana maswala ya afya na Bi. Spika naomba ninukuu kwamba ndani ya Mombasa hii nafikiri baadhi ya zile Wadi ambazo hazina *facilities* ama hospitali moja wapo ni Bamburi. Naona katika hoja hii *paragraph* ya pili anasema, *‘That the Department of Health to establish a prevention and mitigation programme against lifestyle and malignant diseases including awareness campaigns, sensitization forums and other sustainable measures in all Wards’*. Iwapo tutakuwa hatuna hospitali katika Wadi nyengine, basi hili jambo ambalo lasema *sustainable measures* itakuwa tunajidanganya. Kwa hivyo ni bora tunapo hakiki na kuunga mkono Mswada huu tuhakikishe kwamba Kamati ya afya ihakikishe kwamba, *as we are looking forward*, tunapoendelea kuunga mkono tuhakikishe kwamba serikali yetu ya Kaunti iweze kujenga hospitali katika zile Wadi ambazo hazina hospitali na sasa katika Wadi yangu ya Bamburi mara nyingi wanaokuja kunifuata na maswala ya magonjwa kuna wale ambao naweza kuwatajia majina ambao kila wiki lazima nimeanza kushuku labda wengine inaweza kuwa ni maradhi kama haya ambayo hatujui mwanzo wake na mwisho wake.

DISCLAIMER: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor Page 2*

Kwa hivyo naiomba tafadhali Bunge hili kupitia Kamati ya afya iweze kuangalia kwamba hili jambo ambalo wamesema *sustainable measures* iwe ndani yake ni kujenga hospitali katika sehemu kama wadi yangu. Ahsante Bi. Spika na ninaunga mkono Mheshimiwa.

The Temporary Speaker (Hon. Amriya Juma): Thank you Honourable Patrick, yes Honourable Leila?

Hon. Nyache: Ahsante sana Mheshimiwa Spika na mimi kuweza kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia. Kwanza nataka nimshukuru Mwenyezi Mungu. Pili, nimpongeze Mheshimiwa mwenza aliyekuja na hoja hii. Nataka nijulishe Jumba hili ya kwamba hoja hii, Bunge lililopita niliwahi kuleta hoja kama hii ya kuhusiana na ugonjwa wa saratani, na sababu ya kuleta hoja hii Bunge lililopita ni kwa sababu niliuguza jamaa zetu wawili katika familia yetu kwa ugonjwa wa saratani. Mmoja alikuwa ni babangu na mwengine alikuwa ni shangazi yangu. Babangu alikufa na saratani ya koo, na shangazi yangu ya kizazi. Kwa hivyo ikabidi nichukue fursa ya kuweza kuleta hoja hii katika Bunge hili na ilipita isipokuwa kutekelezwa ndio haikutekelezwa. Kwa hivyo vile imefichuliwa tena, ningepomba iweze kutekelezwa. Maoni yangu tu mimi kwa hoja hii ni kusema ya kwamba idara ya afya pamoja na Kamati yetu hapa ya afya waweze kushirikiana na wale madaktari wetu walioko kule mitaani. Tuko na madaktari wale wa Community Health Workers (CHW), wale wanao jitolea katika maswala ya maradhi yoyote, wanazunguka na wana *data* zao katika nyumba zote mitaani wana *data* za magonjwa yote mitaani.

Kwa hivyo ningepomba ikiwa haitatekelezwa kwa haraka maana kujenga hizi zahanati itachukua muda na ikiwa haitaweza kutekelezwa kwa haraka waweze kushirikiana na hawa madaktari wetu wa mitaani ambao wataweza kwenda kuchukua *data* katika majumba ya wale walioko na magonjwa kama haya ya satarani na moyo kwa sababu jamii zetu wengine ni waoga kutoka nje na kwenda kusema ya kwamba mimi nina ugonjwa fulani na wengine nao hawana uwezo wa kwenda hospitali. Kwa hivyo tukishirikiana na wale CHW ambao ni madaktari wa kujitolea, wanaweza kuwapata wale wagonjwa kwa njia ya urahisi na pia tunaweza kusaidia jamii zetu kwa sababu sisi ni viongozi. Hio itakuwa ni njia moja ya kuweza kuwasaidia jamii zetu kule mashinani, wale ambao hawana uwezo wa kuweza kujitibu ama kuweza kutoka nje, hata wale waoga na pia hapo nyuma kulikuwa na mashirika mbalimbali yakizunguka kwa kila Wadi wakija wakipima saratani bure, *free cancer screening* na ilikuwa ikisaidia lakini sasa hivi hakuna. Kwa hivyo pia ningepomba serikali ya Kaunti ikiwa wataweza kufanya jambo hilo pia la kuweza kuzunguka kuleta kile chombo cha kuweza kupima hayo magonjwa hatari ya saratani itakuwa jambo nzuri sana waweze kuingia katika Wadi zote za Kaunti ya Mombasa. Tuweze kusaidia jamii zetu katika maradhi haya ya hatari ya saratani ama maradhi ya moyo. Nimesimama kuunga mkono. Ahsante Mheshimiwa Spika.

The Temporary Speaker (Hon. Amriya Juma): Ahsante Mheshimiwa Leila. Naam Mheshimiwa Pamela?

Hon. Ojala: Thank you Madam Speaker for giving me this time to contribute. First and foremost, I want to congratulate the Honorable Member of Shika Adabu for this Motion. Madam Speaker, as we are all aware that the economy of our country is dilapidated and many people cannot be able to afford this treatment that is why the Honorable Member came with a resolution that sustainable measures must be put in all these Wards so that it will also help our people to minimize the cost of transport and treatment.

Madam Speaker, sorry to mention the name of the Governor of Kisumu, His Excellency Peter Anyang Nyong'o; he has survived with cancer for a long time because he is a wealthy man but what about our people who are very poor, how will they go about this disease Madam Speaker?! So, it is high time I urge the whole House to put this matter into consideration and to see on how we can assist our people because this disease hypertension, diabetes and cancer is a common disease in our county Mombasa and we are supposed to look for remarkable solution on how we can go about it so that our people cannot be affected. Otherwise, I stand to support the motion, Thank you Madam Speaker.

The Temporary Speaker (Hon. Amriya Juma): Thank you Honourable Pamela. Yes Honourable Maryam.

Hon. Baimu: Shukran sana Bi Spika kwa kunipatia nafasi hii. Mimi naunga mkono Mswada huu kwa sababu kusema ukweli huu magonjwa wa saratani, sukari na *hypertension* ni magonjwa ambayo yanasumbua sana watu wetu mashinani. Na tukiangalia haya magonjwa yote matatu ni magonjwa ni *long term* yaani *terminal diseases* mtu ataishi na huo ugonjwa mpaka mwisho wa maisha yake. Kwa hivyo matibabu yake hua yako ghali sana, hivyo basi hivyo itakuwa ni sawa kabisa kama tutafanya hizo kama ni *screening* mashinani ziwe zitafanywa kwa wingi, *sensitization* ziwe zinafanywa raia kuelezwa, kufundishwa juu ya haya maradhi, kuweza kujua vile inanza maanake watu wengi kama hii saratani mwanzo hua ni ngumu sana kutambua kwamba mtu uko nayo mpaka iwe imefika ile *stage* karibu na mwisho kabisa.

Kwa hivyo mimi naunga mkono huu Mswada itakuwa jambo la maana ili katika hizi Kliniki zetu ama hospitali zetu za mashinani iwe zitafanya mambo ya hizi *screening*, Pia kando ya hizi saratani na hizo sukari mimi pia ningependa hizo hospitali zetu za mashinani haswa kama kwangu pale Frere niko na hospitali mbili; Mlaleo na pale Frere kitovuni uwanja, hizo Kliniki ziko lakini madawa hakuna. Kwa hivyo tukiweza kuweka madawa kwa zile Kliniki zetu itakuwa jambo la maana sana, Ahsante sana.

The Temporary Speaker (Hon. Amriya Juma): Yes, Honourable Juma Mwalimu, you can now respond.

Hon. Juma Mwalimu: Ahsante sana Bi. Spika. Mimi nichukue fursa hii kushukuru Waheshimiwa wenza kwa kuunga mkono na kuchangia Mswada huu. Hii yote ni kuashiria wazi kwamba Waheshimiwa wako na imani na kuhurumia wapigaji kura wao kwa sababu ya kupitia majanga ya magonjwa, yangu tu ni kuwapa shukrani na tunaomba Mswada huu uweze kutekelezwa ili wakaazi wetu waweze kupata tiba bora. Ahsante sana Bi. Spika.

The Temporary Speaker (Hon. Amriya Juma): Thank you Honourable Juma Mwalimu. I now put a question that the Motion by Honourable Juma Mwalimu on preventive and mitigation measures against cancer, lifestyle and other malignant disease be approved by this Honourable House in the same terms as moved?

[Question put and agreed to]

The Motion by Honourable Juma Mwalimu on preventive and mitigation measures against cancer, lifestyle and other malignant disease is adopted by this Honourable House. Yes Clerk.

ADJOURNMENT

Honourable Members, this House stands adjourned until Tuesday 14th February, 2023 at 10:00a.m. Thank you.

The House rose at 3:08p.m.